JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU**
**(Limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 8 (1) ya mwaka 2024)**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ambapo jumla ya Shilingi **625,000,000/=** zimetengwa. Hivyo, Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi katika Ofisi za Serikali za Mitaa zilizopo katika maeneo yenu.

**Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo;**

(i) Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na Halmashauri,

(ii) Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali,

(iii) Kikundi cha wanawake na vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenye ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo Timu ya Menejimenti ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa, Halmashauri ya Manispaa Ilemela, 200 Br. ya Buswelu, 33282 Buswelu, S.L.P 735 Ilemela , Mwanza. Simu: + 255 (28) 2981196, Nukushi: + 255 (28) 2981196,
Barua pepe: md@ilemelamc.go.tz Tovuti: www.ilemelamc.go.tz
*(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa)*

CamScanner

wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine,

(iv) Kikundi kiwe na Akaunti ya Benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali; na

(v) Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye akili timamu na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa kuwa na wanakikundi wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45. Wawe na namba za Nida.

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielektroniki (tembelea tovuti: mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa kata husika au Mtendaji wa Kata husika.

***Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo;***

- ✓ Barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa Mtaa
- ✓ Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo
- ✓ Andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo ndani ya mfumo na taarifa ya Akaunti ya Benki.

***NB: Vikundi vya Vijana na watu wenye ulemavu vitapewa kipaumbele zaidi iwapo watakidhi vigezo vilivyoainishwa.***

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni **Tarehe** 19 **Mwezi** 12 **Mwaka** 2025

Tangazo hili limetolewa na: -

Ummy M. Wayayu
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**ILEMELA**

MKURUGENZI HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA S.L.P 735 MWANZA

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa, Halmashauri ya Manispaa Ilemela, 200 Br. ya Buswelu, 33282 Buswelu, S.L.P 735 Ilemela , Mwanza. Simu: + 255 (28) 2981196, Nukushi: + 255 (28) 2981196,
Barua pepe: md@ilemelamc.go.tz Tovuti: www.ilemelamc.go.tz
*(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa)*

CamScanner